# STANDARD 6 KISWAHILI
# MID-TERM 1 2020

*MUDA: Saa1 dakika 40*

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lililo sahihi.***

Nzige ni wadudu wanaopaa wanaofanana na __1__. Wadudu hawa ni waharibifu sana __2__ mimea. __3__ hutembea katika makundi. Kundi la nzige linapokuwa mbali angani huonekana __4__ wingu kubwa la mvua.

Nzige wanapovamia mashamba hula __5__ yote na kuiacha mimea __6__ imebaki na vijiti tu. __7__ ya haraka isipochukuliwa, wakulima wanaweza kupata hasara kubwa kwa kuharibiwa mimea. __8__ uharibifu wa mimea waweza kugeuka kuwa janga la njaa __9__ kitaifa. __10__ basi nzige wanapovamia sehemu __11__ ya nchi, serikali huanzisha vita au harakati za __12__ nao. Serikali hutumia mbinu __13__ kuwanyunyizia kemikali __14__ kuwaangamiza. Mbinu __15__ hujumuisha hata matumizi ya ndege angani.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. nyuki | B. nzi | C. panzi | D. mbu |
| 2. | A. na | B. kwa | C. kuwa | D. ni |
| 3. | A. Wao | B. Wale | C. Hao | D. Hawa |
| 4. | A. pia | B. na | C. bila | D. kama |
| 5. | A. matawi | B. majani | C. mizizi | D. magome |
| 6. | A. wakati | B. ambapo | C. ikiwa | D. iwapo |
| 7. | A. Sheria | B. Njia | C. Sababu | D. Hatua |
| 8. | A. Nao | B. Bali | C. Wala | D. Lakini |
| 9. | A. wa | B. la | C. ya | D. cha |
| 10. | A. Pia | B. Nayo | C. Ndiyo | D. Hivyo |
| 11. | A. wowote | B. lolote | C. yoyote | D. zozote |
| 12. | A. kupambana | B. kupigana | C. kuelewana | D. kushindana |
| 13. | A. yote | B. lote | C. zote | D. wote |
| 14. | A. bila | B. ili | C. ila | D. hata |
| 15. | A. hii | B. hiki | C. hili | D. hizi |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo.***

16. Ni sentensi ipi iliyotumia kirejeshi **'ndi'** kwa usahihi?
   A. Sisi ndio tuliojenga nyumba hii.
   B. Sisi ndiye tuliojenga nyumbani hii.
   C. Sisi ndisi tuliyejenga nyumba hii.
   D. Sisi ndisi tuliojenga nyumba hii.

17. Ni sentensi ipi inayoonyesha **'ki'** ya masharti?
   A. Kitabu kilichopotea kimepatikana.
   B. Amevaa mavazi ya kifalme.
   C. Ukishinda utatuzwa zawadi.
   D. Kibanda shetu kitabomolewa.

18. Ni nomino gani haitokani na neno **'lima'**
   A. kilimi
   B. ukulima
   C. kilimo
   D. mkulima

19. Ni sentensi gani haikutumia kirejeshi **-ote** kwa usahihi.
   A. Tunda lote limeoza.
   B. Maji yote yamemwagika.
   C. Nguo zote zimeibwa.
   D. Tutaenda sisi wote.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**20.** Ni sentensi gani iliyotumia **'karibu'** ya kuonyesha nusura.
A. Kwao ni karibu na kwetu.
B. Alijikwaa karibu aanguke.
C. "Karibu mgeni," Mama alisema.
D. Usicheze karibu na moto.

**21. Tumia kivumishi kimilishi kwa usahihi:**
Gari __________ limeharibika.
A. yangu B. langu
C. wangu D. changu

**22. Iandike sentensi hii ukitumia 'amba' rejeshi:**
"Mtoto aliyepotea amepatikana."
A. Mtoto ambaye atapotea atapatikana.
B. Mtoto ambaye aliyepotea amepatikana.
C. Mtoto ambaye alipotea amepatikana.
D. Mtoto ambaye alipotea alipatikana.

**23. Kanusha sentensi ifuatayo:**
Wewe utaenda shuleni.
A. Wewe hutaenda shuleni.
B. Wewe huendi shuleni.
C. Wewe hautaenda shuleni.
D. Wewe hukwenda shuleni.

**24.** Neno ugonjwa liko katika ngeli gani?
A. LI - YA
B. U - ZI
C. U - U
D. U - YA

**25.** Ni kitenzi kipi kinachoonyesha kauli ya kutendeana
A. pigana B. pigiana
C. pigisha D. pigapiga

**26.** Ni sentensi gani iliyoakifishwa vizuri.
A. Niletee vitu vifuatavyo, kitabu, kalamu na rula.
B. Niletee vitu vifuatavyo: Kitabu, kalamu, na rula.
C. Niletee vitu vifuatavyo kitabu, kalamu na rula.
D. Niletee vitu vifuatavyo: Kitabu, kalama na rula.

**27. Kamilisha kwa usahihi:**
Tunasema kuwa barabara imenyooka _____
A. twaa! B. rwaa!
C. nywee! D. ndi!

**28. Kamilisha methali ifuatayo:**
Mwenye nguvu __________
A. mwache B. mwogope
C. mpishe D. mpige

**29.** Ni mnyama gani hakulinganishwa kwa usahihi na kikembe chake?
A. Sungura - Kitungule
B. Simba - Shibli
C. Chui - Kiluwiluwi
D. Ng'ombe - Ndama

**30. Andika tarakimu ifuatayo kwa maneno:**
10,001
A. Elfu moja na moja.
B. Elfu kumi na moja.
C. Kumi na moja elfu.
D. Kumi elfu na moja.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Neno 'mshenzi' linapotajwa watu wasiojua maana yake hudhani kuwa ni matusi mabaya sana. Unapomwita mtu mshenzi, kwa mfano, mtu huyo hukasirika na kuzua vita akidhani kuwa umwemwita mjinga ama mpumbavu. Lakini neno mshenzi halimaanishi mjinga wala mpumbavu. Mshenzi ni mtu asiyekuwa na tabia za kistaarabu au kiungwana. Mshenzi ni mtu fidhuli, mkali na katili - mwenye tabia zisizokuwa za kiutu.

Kinyume na mshenzi, mstaarabu ni mtu mpole na mwenye heshima kwa binadamu wenzake. Ni mtu mwenye adabu na utu. Yeye huwasikiliza na kuwaelewa wengine.

Ushenzi na ustaarabu hudhihirika katika tabia zetu. Mtu mshenzi ana tabia na matendo yanayoudhi. Si mtu anayejua kuomba msamaha wala kusikitikia matendo yake maovu. Si mtu anayependa maelewano wala amani. Naye mtu mstaarabu ni yule anayefuata na kuzingatia maadili mema katika jamii. Ana heshima kwa wakubwa na wadogo. Si jeuri wala fidhuli, ni mpole kwa binadamu wenzake. Lugha yake ni ya heshima na adabu. Anajua kuomba msamaha anapokosea na kutafuta suluhu kwa njia ya amani anapokosewa. Bila shaka dunia ingekuwa mahali pa amani kama ingejawa na watu wastaarabu.

Lakini tunawezaje kuendelea na kufikia ustaarabu wa hali ya juu? Jambo la kwanza ni lazima tuzingatie maadili ya kifamilia tunayopewa na wazazi wetu. Pili tuzingatie ushauri na maelekezo tunayopewa na walimu



**Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748**
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

wetu na muhimu zaidi tuzingatie mafundisho mema ya kidini, kwani Mungu ndiye chanzo cha maadili yote mema.

Tusisahau maneno ya maana kama vile tafadhali, samahani, niwie radhi, naomba, pole na asante. Hivyo ndivyo viungo muhimu katika kujenga tabia njema za kistaarabu na kiungwana. Tabia za kistaarabu ndizo huondoa ushenzi na kumtofautisha binadamu na mnyama. Ndizo pia humfanya binadamu kuwa na utu; na utu ndio humfanya binadamu kuwa mtu. Binadamu asipokuwa na utu ni mnyama ingawa ni mtu ni mnyama wa miguu miwili.

**31.** Neno 'mshenzi' linapotajwa, watu hudhania mambo yafuatayo isipokuwa
A. ni matusi mabaya sana.
B. ni mtu mstaarabu.
C. ni mjinga.
D. ni mpumbavu.

**32.** Ni tabia gani kati ya hizi zimetajwa kuwa za kishenzi.
A. Ufidhuli, ukali, ukatili.
B. Ufidhuli, upole, ukatili.
C. Ustaarabu, upole, ungwana.
D. Ukali, ukatili, upole.

**33.** Ni gani kati ya hizi si tabia za kistaarabu.
A. Upole B. Heshima
C. Adabu D. Ufidhuli

**34.** Ushenzi na ustaarabu hudhihirikaje kulingana na hadithi?
A. Katika nyuso zetu.
B. Katika maumbile yetu.
C. Katika tabia zetu.
D. Katika mioyo yetu.

**35.** Matendo ya mtu mshenzi ________
A. yanaudhi B. yanafurahisha
C. yanapendeza D. yanachangamsha

**36.** Mtu mshenzi hawezi kufanya mambo yafuatayo isipokuwa moja. Ni lipi?
A. Kuomba msamaha.
B. Kupigana na kutusiana.
C. Kusikitikia matendo yake maovu.
D. Maelewano na amani.

**37.** Kulingana na hadithi dunia ingekuwa na ________ kama ingejawa na watu wastaarabu.
A. utu B. umoja
C. upendo D. amani

**38.** Ni jambo gani lisilotusaidia kufikia ustaarabu wa hali ya juu?
A. Maadili ya kifamilia.
B. Tamaduni zisizofaa.
C. Ushauri wa walimu.
D. Mafundisho ya kidini.

**39.** Mwandishi anasema kuwa ni nani ndiye chanzo cha maadili yote mema?
A. Mungu B. Mzazi
C. Mwalimu D. Dini

**40.** ________ ndio humfanya binadamu kuwa mtu.
A. Ustaarabu B. Ungwana
C. Utu D. Tabia njema

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.***

Ole Sankara alikuwa ni shujaa miongoni mwa jamii ya Wamaasai. Yeye alikuwa mtu jasiri asiyeogopa chochote. Akiwa machungani aliweza kukabiliana na simba waliojaribu kushambulia mifugo wake na kuwaua. Hata simba walipomwona walimheshimu na kumwondokea. Wanakijiji walishangazwa na ujasiri wake usio wa kawaida.

Siku moja wahudumu wa afya walitembelea kijijini mwao. Walikuwa wakipiga mbiu wakitangaza kuwa kulikuwa na maadui hatari waliokuwa wamevamia kijiji chao. Waliwashauri watu wajikinge na maadui hao kwa kulala ndani ya vyandarua.

Ole Sankara alijawa na shauku ya kutaka kujua maadui hao ni akina nani. Na ni kwa nini watu walishauriwa kulala ndani ya vyandarua badala ya kulala tu ndani ya nyumba na kufunga milango. "Mbu ni adui hatari," mhudumu wa afya aliendelea "wanapokushambulia na kukuuma wanaweza kukuambukiza ugonjwa wa maleria; nayo malaria huua. Malaria ndiye muuaji nambari moja dunia-ini. Huua mamilioni ya watu kila mwaka."

"Mbu?" Ole Sankara alishangaa. "Mdudu mdogo kama mbu anawezaje kunitisha? Mimi Ole Sankara nimepambana na wanyamapori kama vile chui, duma hata simba; nawezaje kutishwa na mdudu mdogo kama



**Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748**
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

bu?" Ole Sankara alijuliza.

Ole Sankara alipuuzilia mbali ushauri wa wahudumu wa afya na kuuona kama mzaha tu. Aliwakejeli a kuwachekelea wale waliolala ndani ya vyandarua.

"Wacha nione mbu wakinikaribia," alisema Ole Sankara. "Watajua mimi ni Ole Sankara muua simba." Majuma kadhaa yalipita Ole Sankara akishikilia msimamo wake.

Siku moja Ole Sankara aliamka asubuhi viungo vyake vya mwili vikiwa vimelegea. Alijihisi mchovu iasi. Alijikaza na kuendelea na shughuli zake za kawaida, akidhani kuwa ulikuwa tu uchovu wa kawaida. Aliwapeleka ng'ombe machungani ilivyokuwa desturi yake.

Jioni alirejea nyumbani akitetemeka kwa baridi. Alijifunika kwa blanketi akidhani kuwa ilikua baridi ya kawaida. Usiku joto la mwili lilipanda. Alitokwa na jasho hadi blanketi likalowa kana kwamba lilimwagiwa maji. Hapo ndipo Ole Sankara alipotambua kuwa hali yake haikuwa ya kawaida.

Asubuhi na mapema, akisindikizwa na mke wake, Ole Sankara alizuru kituo cha afya kilichokuwa karibu. Aliwakuta wahudumu wale wale wa afya aliowaona kijijini mwao. Walimshughulikia kwa haraka na kuyanusuru maisha yake. Hapo ndipo Ole Sankara alipojifunza kuwa usimdharau mtu kwa sababu ya udogo wake wa kimaumbile.

**41.** Taja hulka ya Ole Sankara kutokana na aya ya kwanza.
A. Jasiri
B. Mzembe
C. Mwoga
D. Goigoi

**42.** Simba walipomwona Ole Sankara
A. walimkejeli na kumdharau.
B. walimkimbilia na kumshambulia.
C. walimheshimu na kumwondokea.
D. walimkaribia na kumrambaramba.

**43.** Watu walishauriwa wajikinge na adui kwa kulala wapi?
A. Ndani ya mapango.
B. Ndani ya vyandarua.
C. Ndani ya nyumba.
D. Juu ya meli.

**44.** Kulingana na mhudumu wa afya mbu huua watu wangapi?
A. Mamia ya watu.
B. Maelfu ya watu.
C. Makumi ya watu.
D. Mamilioni ya watu.

**45.** Kati ya wanyamapori Ole Sankara amewahi kupambana nao ni yupi hakutajwa?
A. Chui
B. Nyati
C. Duma
D. Simba

**46.** Ole Sankara aliwafanyia nini waliolala ndani ya vyandarua.
A. Aliwakejeli na kuwachekelea.
B. Aliwadharau na kuwatukana.
C. Aliwaheshimu na kuwasifu.
D. Aliwapuuza na kuwaepuka.

**47.** Kulingana na hadithi Ole Sankara alishikilia msimo wake kwa muda gani?
A. Miezi kadhaa
B. Siku kadhaa
C. Miaka kadhaa
D. Majuma kadhaa

**48.** Ole Sakara aliporejea nyumbani jioni alikuwa ____________
A. amelegea viungo vya mwili.
B. akitokwa na jasho.
C. akitetemeka kwa baridi.
D. katika hali ya kawaida.

**49.** Ole Sankara alizuru kituo cha afya wakati gani?
A. Usiku
B. Mchana
C. Asubuhi
D. Jioni

**50.** Ni kichwa gani kinachofaa hadithi hii?
A. Shujaa Ole Sankara.
B. Mbu-adui hatari.
C. Wahudumu wa afya.
D. Simba - mnyama hatari.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com